**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA SHULE**
**YA SEKONDARI YA NASIBUGANI**

*"Barua zote zielekezwe kwa Mkuu Wa Shule"*

**Simu: 0689890032**
**0672149188**

**Mkuu wa Shule,**
**S.L.P, 06,**
**Mkuranga.**

**Email: nasibugani.secondaryschool@mkurangadc.go.tz**

---

**Kumb Na. NSS /F V/SEC/VOL.1/…..**
Mzazi / Mlezi wa…………………………………….
S. L. P………………………
……………………………...

**YAH: TAARIFA YA MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA ………… SHULE YA SEKONDARI NASIBUGANI**

## 1.0 UTANGULIZI

Bodi ya shule, walimu, wafanyakazi na wanafunzi wa shule ya sekondari Nasibugani wanakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka **………. Tahsusi ya CBG/HGL/HGLi ……..** na wanakukaribisha katika shule hii. Ni imani yetu utaitumia nafasi hii adimu kusoma na kujifunza kwa bidii na kwa uwezo wako wote pamoja na kushirikiana na wenzako, walimu na jumuiya nzima ya Nasibugani ili kulinda heshima na sifa ya shule kwa maendeleo ya yako na Taifa letu.

## 2.0 MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Nasibugani ipo katika kijiji cha **Nasibugani**, kata ya **Msonga**, tarafa ya **Kisiju**, Wilaya ya **Mkuranga** mkoa wa **Pwani**. Umbali wake ni km **48** kutoka makao makuu ya Wilaya ya Mkuranga upande wa mashariki jirani na bahari ya Hindi.

Usafiri wa mabasi unaanzia **Mbagala rangi tatu (STENDI YA SHAMBA), Dar–esSalaam** kupitia barabara kuu ya **Kilwa Road** iendayo mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara hadi kijiji cha **Nyamalonda (Mita chache baada ya viwanda vikubwa kioo cha Sapphire na Kiwanda cha Tiles cha GoodWill)** na kufika eneo la Kijiji cha **Msonga** ambapo utapanda pikipiki kufika shuleni. **(TUMIA NJIA HII KUTOKANA NA CHANGAMOTO YA MVUA KUHARIBU MIUNDOMBINU YA NJIA YA KUTOKA BARABARA YA KISIJU KUFIKA SHULENI)**

Lakini Pia usafiri unapatikana eneo la **Mbagala rangi3** kuelekea **Kisiju Pwani**, utashukia kituo cha **Mavunja** unakunja upande wa kulia. Tunashauri kabla ya kuanza safari ukitokea **Mbagala**, hakikisha unawasiliana na uongozi wa shule kwa namba zilizowekwa katika fomu hii ili usipotoshwe.

## 3.0 KICHOKOO CHA SHULE "SCHOOL MOTTO"

Kichokoo cha shule (school motto") cha shule ya sekondari **Nasibugani** ni **"ELIMU NI UKOMBOZI" (EDUCATION IS LIBERATION)**. Ukiwa mwanafunzi wa shule hii

tunatarajia utakuwa na nidhamu ya hali ya juu itakayokuwezesha kujijenga kitaaluma na ufanisi mkubwa na hivyo kwa kujikomboa kimaisha na kuwa mtaalamu / raia mwema wa Taifa la kesho.

**4.0 MAHITAJI YA SHULE**

**A. SARE ZA SHULE**

**WAVULANA**

i. Suruali mbili za dark blue (zenye marinda mawili mbele kila upande) na tai zinayofanana na rangi ya suruali. (Aje nazo mwanafunzi mwenyewe)

ii. Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu (Aje nazo mwanafunzi mwenyewe)

iii. Suruali za kaki mbili moja akiwa ameivaa pamoja na tshirt ya kijivu ambayo haina kola. Atakuwa anavaa suruali hizo siku ya Jumamosi, Jumapili na wakati wote usio wa masomo. (**Mwanafunzi asije shuleni na nguo ambazo hazijaainishwa katika maelekezo haya.**)

iv. Mwanafunzi aje na fulana ya kijivu (Tshirt yenye kola) ambayo itawekwa nembo ya shule kwa ajili ya matumizi ya mbadala wa uniform siku za Jumatano na Ijumaa.

v. Mkanda mweusi, viatu vyeusi vyenye visigino vifupi (gidamu) soksi nyeusi jozi mbili, sweta ya rangi dark blue yenye msuko wa **V** mbele, nguo za michezo (Track suit za dark blue na jezi za dark blue pamoja na raba ya mazoezi)

vi. Lazima kuja na chandarua, shuka mbili za light blue, mto, foronya, ndoo mbili ndogo za lita 10, Sahani, Bakuli, kikombe, kijiko na vifaa vingine vya usafi wa mwili. Unaweza kuvinunua Mbagala ili kupunguza usumbufu. (Havipatikani eneo la shule)

vii. Kila mwanafunzi aje na godoro jipya lenye upana wa **futi 2.5**. (**Magodoro yaliyotumika yachukuliwe kwa tahadhari, ili kuepuka wadudu wasumbufu kama kunguni na chawa).**

viii. Kila mwanafunzi anapaswa kuja na" SPRING ***FILE"*** kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake za muhimu.

**5.0 MAHITAJI MENGINE MUHIMU SANA**

**A) MICHANGO YA SHULE**

| NA | MAELEZO | KIASI |
|---|---|---|
| **i.** | Gharama za uendeshaji wa shule | 65,000 |
| **ii.** | Kitambulisho cha shule | 6,000 |
| **iii.** | Nembo ya shule | 4,000 |
| **iv.** | Tahadhari | 5,000 |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Tanbihi**

- Fedha yote ilipwe **BENKI** kwenye akaunti ya shule **NMB A/C NO. 20701200159** jina la akaunti ni **SHULE YA SEKONDARI NASIBUGANI. Hakikisha unaandika Jina kamili la mwanafunzi sehemu ya mlipaji.**
- Hatupokei fedha taslimu, pia hakikisha unakuja na nakala ya hati ya malipo shuleni.

**B) BIMA YA AFYA**

Jukumu la matibabu ni la mzazi/mlezi, hivyo unashauriwa kuhakikisha mwanafunzi wako ana bima ya afya ya Taifa (**NHIF**) au mfuko mwingine wowote unaotambuliwa na serikali. ***Kila mwanafunzi ni lazima aje na bima ya afya ya NHIFau CHF.***

## 6.0 VIFAA VYA DARASANI

a) Daftari kubwa 'counter books' 10 au zaidi
b) Mkebe wa hisabati na kikokotozi kwa tahasusi ya **CBG**, **HGL** na **HGL**i
c) Advanced learner's dictionary moja, rula yenye cm 30, kalamu za wino na penseli za kutosha.
d) Vitabu vya masomo vinavyo endana na Tahasusi yako.
e) Bunda la karatasi (ream A4) mbili kwa mwaka (utakabidhi).
f) **KOTI JEUPE LA MAABARA** kwa wanafunzi wa **CBG**
g) **DISSECTING KIT** kwa wanafunzi wa **CBG**

## 7.0 VIFAA VYA KAZI

I. Kwa wanafunzi wa **CBG**, Aje na **Kwanja , jembe, soft bloom,** na **Squeezer .**
II. Kwa mwanafunzi wa **HGL** na **HGLi** Aje na **Jembe lenye mpini** , **Hard Bloom** , **jembe**, na **panga**

## 8.0 SHERIA ZA SHULE

**Nidhamu kwa ujumla**

1. Ni lazima Mwanafunzi awahi shuleni asubuhi saa 1:00 na kufanya usafi wa mazingira ya shule na kuhudhuria gwaride la ukaguzi na kuchangamsha mwili.
2. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuondoka katika eneo la Shule bila kupata kibali kutoka kwa Mwalimu wa darasa, Mwalimu wa zamu au Idara ya Malezi.
3. Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kusalimia na kuwapokea mzigo Walimu au mtu yeyote mwenye umri mkubwa zaidi yake popote akutanapo na watu aina hiyo.
4. Hairuhusiwi kutumia **LUGHA CHAFU** miongoni mwa Wanafunzi na kwa mtu mwingine yeyote.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu Wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote wa shule.
6. Kila Mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na shughuli za michezo na uzalishaji mali kwa mujibu wa ratiba.
7. Mwanafunzi lazima afanye mitihani ya masomo yote anayosoma shuleni hapa.
8. Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kuwa na aina yoyote ya vitu vifuatavyo:- Kucha ndefu, kupaka rangi, kuvaa cheni, hereni, nywele ndefu, kunyoa kipara, kunyoa nyusi, kupaka dawa nywele, n.k.
9. Mwanafunzi ahakikishe kuwa awapo mahali popote ndani au nje ya shule awe amevaa nguo za heshima, ni marufuku kuvaa zinazobana, fupi na nyepesi.
10. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo zaidi ya zile zilizotajwa katika maelezo ya kujiunga na shule, ikiwemo sweta la rangi inayotakiwa.
11. Wanafunzi wanatakiwa kutunza mali zao binafsi na mali za Shule. Pia wanatakiwa kutoa taarifa kwenye utawala juu ya uharibifu wa mali ya Shule.
12. Ni marufuku kwa Mwanafunzi kukutwa sehemu zifuatazo:-
    (i) Baa na klabu za usiku.
    (ii) Nyumba za kulala wageni isipokuwa wanapokuwa na wazazi au walezi wao.
13. Wawapo shuleni Wanafunzi hawaruhusiwi kumiliki vitu vya gharama kama simu ya mkononi, Redio, Kamera, Ipad, Albam za picha na CD.
14. Hakikisha ukimya wa hali ya juu unazingatiwa katika maeneo yote ya shule na yakujifunzia hasa Darasani, Maktaba, Maabara na kwenye karidos wakati wa vipindi.
15. Hakikisha muda wote unapokuwa shuleni unaongea lugha ya kiingereza nje na ndani ya darasa.

16. Mwanafunzi yeyote akikamatwa na kitu chochote kisichotakiwa shuleni kitaharibiwa mbele yake.

**A. MAKOSA AMBAYO MWANAFUNZI AKIYAFANYA ANAWEZA KUFUKUZWA SHULE**

1. Ulevi au matumizi ya madawa ya kulevya.
2. Aina zote za wizi au unyang'anyi.
3. Aina zote za makosa ya kujamiiana na uasherati. Hii ni pamoja na kukutwa na mikanda ya video, vitabu vichafu vya uasherati au vitu vinavyofanana na hivyo.
4. Kupiga na kupigana.
5. Matumizi ya lugha chafu au matusi.
6. Makosa ya jinai.
7. Kuzomea watu au kuchokoza wanafunzi wengine.
8. Kugoma au kuchochea mgomo (ghasia).
9. Kutohudhuria shuleni kwa muda wa siku 30 mfululizo bila taarifa.
10. Kudharau bendera ya Taifa kwa kutohudhuria paredi.
11. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule, (Pia ikithibitiha kutoa mimba).
12. Kuoa au kuolewa.
13. Kukuwadia Mwanafunzi mwenziwe na mtumishi yeyote katika mambo ya mapenzi ndani na nje ya Shule.
14. Kunyanyasa Mwanafunzi mwenzie kutokana na jinsia yake, udini, ulemavu, ugeni wake au hali yake.
15. Kughushi mitihani au wizi wa mitihani, kukataa au kutofanya mitihani na mazoezi ya masomo bila sababu za msingi.
16. Kukataa adhabu kwa makusudi. Pia adhabu inaweza kutolewa na Mwalimu au Kiranja yeyote kwa mwanafunzi anayeonesha utovu wa nidhamu.
17. Kuharibu mali ya shule ikiwa ni pamoja na majengo, mali ya mtu au kundi la watu.
18. Kukamatwa na simu, redio, kamera, Ipad, Albam za picha na CD kwa mara ya pili baada ya kuonywa kwa mara ya kwanza.

**MWISHO**

a) Wanafunzi wanapaswa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **…………….** hadi tarehe **…………….** ili kuleta ufanisi kwenye kalenda ya masomo
b) **SIMU PAMOJA NA NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI. KABLA YA KURUHUSIWA KUINGIA BWENINI UTAPEKULIWA**
c) Unatakiwa kuja na nakala ya "**Result slip**" yako ya kidato cha nne na nakala ya cheti cha kuzaliwa.
d) **Zingatia:** Mwanafunzi aje shule akiwa amevaa suruali ya kaki na Tshirt ya kijivu isio na kola na isiokua na maandishi yoyote (mikono mifupi)
e) Hakikisha una pima afya yako kwenye hospitali inayotambulika na serikali.
f) Kwa mawasiliano piga simu

**0689890032 / 0672149188 --Mkuu wa Shule**
**0653392543 – Makamu Mkuu wa Shule**
**0685720073 – Mwalimu wa Taaluma**

**NB: Tunaomba wazazi kulipa michango kwa wakati ili kuendana na Taratibu za kibajeti za serikali.**

# Karibu Sana Shule Ya Sekondari Nasibugani

**……………………………..**
**SHUKRANI R. KOTI**
**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA**
**SHULE YA SEKONDARI NASIBUGANI**
**Simu +255784339372 AU +255686960900** **Ofisi ya Mkuu wa shule,**
**Barua pepe** nasibuganihighschool@gmail.com**:** **S . L . P 6, Mkuranga.**

Kumb No. NSS/F.V/2023./Vol.01
Tarehe ………………………..

***PICHA YA MWANAFUNZI***

**YAH: FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)**

**SEHEMU A: (** *IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE*)

1. Jina kamili la mwanafunzi (***majina matatu***) ………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa (***Siku/Mwezi/ Mwaka***)……………………………………………......
3. Mahali alipozaliwa (***kijiji/wilaya/mkoa***) …………………………………………………..
4. Uraia …………………………………………………….
5. Dini ……………………………………………………….
6. Dhehebu …………………………………………….....
7. Shule ya sekondari aliosoma ……………………………………………………………
8. Namba ya Mtihani ……………………………………………………………………..
9. Mahali unakotoka (kijiji/ wilaya/ mkoa) ………………………………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi ____________________________________________ Nikiwa na akili zangu timamu bila kushurutishwa ama kulazimishwa na mtu yeyote ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha Tano. "***Ninaahidi kutii kikamilifu sheria, taratibu na kanuni zote za shule wakati wote niwapo mwanafunzi wa SHULE YA SEKONDARI NASIBUGANI .***"

**Sahihi ya mwanafunzi**……………………**Sahihi ya mzazi**....................... **TAREHE** …………………

**SEHEMU "B" – (**IJAZWE *NA MZAZI/MLEZI***)**

1. Jina la Mzazi/ mlezi …………………………………………
2. Kazi yako ……………………………………………….....
3. Anuani/Simu ……………………………………………......
4. Mahali unapoishi ……………………………………………
5. Namba ya NIDA …………………………………………….

***PICHA YA MZAZI/MLEZI***

**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA**
**SHULE YA SEKONDARI NASIBUGANI**
**Simu +255784339372 AU +255686960900** **Ofisi ya Mkuu wa shule,**
**Barua pepe** nasibuganisecondaryschool@gmail.com**:** **S . L. P 6, Mkuranga.**

***PICHA YA MWANAFUNZI***

---

Kumb No. NSS/F.I/20…/Vol.01
**YAH: FOMU YA TAARIFA YA AFYA YA MWANAFUNZI** (*Medical Examination Form*)
**Maelezo:** Fomu hii ijazwe na Daktari wa Hospital inayotambulika na Serikali (Hospitari za Serikali).
Mimi (Jina la Daktari) ____________________________________________
Nathibitisha kuwa mwanafunzi (Jina la mwanafunzi) ________________________________________
Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana ana/hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:-

**A. Hali ya mwili**

- ✓ Mapigo ya moyo ……………………………………………………………..........
- ✓ Haemoglobin ……………………………………………………………
- ✓ Kundi la damu (blood group)…………………………………………
- ✓ Mkojo …………………………………………………………………………
- ✓ Kinyesi ……………………………………………………………………
- ✓ Macho yana kasoro ……………………………………………………………
- ✓ Masikio yana kasoro …………………………………………………

**Angalia ;** Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa A.

**B. Magonjwa.**

- ✓ Bronchial asthma ……………………………………………………… ☐ Tuberculosis ………………………………………………………… ☐ Epilepsy ……………………………………………………………………..
- ✓ Blood pressure …………………………………………………………………
- ✓ Peptic/duodenal ulcers …………………………………………………………
- ✓ Sickle cell ……………………………………………………………………
- ✓ Venereal diseases [give type] …………………………………………………
- ✓ Mental illness ………………………………………………………………
- ✓ HIV/AIDS ……………………………………………………………………

JINA LA DAKTARI ………………………..............................
SAINI ………….................
MHURI……………..
TAREHE ………………